**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FUNGU 44 KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

*[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025]*

Idara ya Kamati za Bunge,
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P. 941,
**40490 DODOMA.**

**22 Mei, 2026**

# YALIYOMO

**Ukurasa**


**ORODHA YA MAJEDWALI** .................................................................... ii
**SEHEMU YA KWANZA** .................................................................... 1
**1.0 MAELEZO YA JUMLA** .................................................................... 1
1.1 Utangulizi .................................................................... 1
1.2 Msingi wa Taarifa .................................................................... 2
1.3 Mawanda ya Uchambuzi .................................................................... 3
**SEHEMU YA PILI** .................................................................... 4
**2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/ 2026** .......................... 4
2.1 Ufafanuzi wa Jumla .................................................................... 4
2.2 Uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. .................................................................... 5
2.2.1 Taarifa ya Fedha zilizovuka Mwaka 2024/2025..... 5
2.2.2 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida .. 6
2.2.3 Upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo. . 8
2.2.4 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo . 12
2.2.5 Hali ya Uzingatiaji wa Ushauri Uliotolewa na Kamati 14
**SEHEMU YA TATU** .................................................................... 16
**3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** ................................................ 16
3.1 Makadiriro ya Matumizi ya Kawaida ............................ 16
3.2 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ....... 19
**SEHEMU YA NNE** .................................................................... 22
**4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI** .......................................... 22
**SEHEMU YA TANO** .................................................................... 28
**5.0 HITIMISHO** .................................................................... 28
5.1 Maelezo ya Kuhitimisha .................................................................... 28

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali Na. 1:** Fungu 44 Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida 2025/2026 ....................6

**Jedwali Na. 2:** Fungu 44 - Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ....................9

**Jedwali Na. 3:** Ulinganisho wa Fedha za Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na 2026/2027 ....................17

**Jedwali Na. 4:** Ulinganisho wa bajeti ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na2 026 na 2027 ....................19

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, **Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla ili kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;
(b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti wa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
(c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

(d) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na

(e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

## 1.2 Msingi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa taarifa hii unatokana na majukumu ya Kamati ambayo yapo kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1)(a) na Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 121 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hizo kwa pamoja zimeweka masharti yanayohusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekekezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Kwa masharti hayo, Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ilifanya uchambuzi na kupata maudhui ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na uchambuzi huo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Bunge yanayohusu kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Kazi hiyo ilifanyika kuanzia ya tarehe 12 hadi 14 Machi 2026 katika Mikoa ya Dar Es Salaam na Pwani. Napenda kulijulisha Bunge lako

Tukufu kuwa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ulitumia matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Viwanda na Biashara.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara inagusa **Fungu 44** ambayo ni Wizara yenyewe ikiambatana na baadhi ya taasisi zilizo chini ya wizara hiyo. Naomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa fungu hilo tarehe 24 na 26 ya Mwezi Machi 2026.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/ 2026

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Katika vikao vya Kamati vilivyoketi tarehe 24 na 26 ya Mwezi Machi, 2026. Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara **(Fungu 44)** zilizohusu pamoja na mambo mengine Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hiyo umeangazia maeneo makuu manne ambayo ni;

(a) Taarifa ya fedha zilizovuka Mwaka wa Fedha 2024/2025

(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya kawaida na Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari 2026;

(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni uliotolewa na Bunge wakati wa kujadili Makadirio

ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** mambo hayo yanatoa taswira muhimu kwa Bunge kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## 2.2 Uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara inajumuisha fungu moja – **Fungu 44.**

### 2.2.1 Taarifa ya Fedha zilizovuka Mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Viwanda na Biashara (**Fungu 44**) iliomba kibali cha kuvuka na jumla ya **Shilingi 2,323,391,970** ili kutekeleza kazi mbalimbali za maendeleo katika miradi yake miwili inayosimamiwa na SIDO na CAMARTEC,kati ya fedha hizo **Shilingi 1,752,821,741** ni kwa ajili ya SIDO na **Shilingi 570,570,229** ni kwa ajili CAMARTEC**.** Hadi kufikia Februari 2026, **Shilingi 885,173,570** zilitumika na **Shilingi 1,438,214,400** zilikuwa bado hazijatumika kutokana na taratibu mbalimbali za manunuzi kuendelea.

### 2.2.2 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida


**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Viwanda na Biashara - **Fungu 44** iliidhinishiwa **Shilingi 93,900,697,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 18,081,317,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 75,819,380,000.00** ni kwa ajili ya mishahara.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Mwezi Februari, 2026 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 58,704,127,320.73** sawa na asilimia **62.5** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 47,672,881,443.79** sawa na asilimia **62.9** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 11,031,245,876.94** sawa na asilimia **61.0** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 1**

Jedwali Na. 1: Fungu 44 Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida 2025/2026

| **Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya kawaida kwa Mwaka 2025/2026 - Fungu 44** | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Kilichoidhinishwa** | **Kilichopokelewa** | **Asilimia** |
| Mishahara | 75,819,380.000 | 47,672,881,443.79 | 62.9 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 18,081,317,000 | 11,031,245,876.94 | 61.00 |
| **Jumla Kuu** | **93,900,697,000** | **58,704,127,320.73** | **62.5** |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara 2026/2027*-Fungu 44 na usanifu wa Kamati




**Chanzo:** *Randama ya Wizara 2026/2027*-Fungu 44 na usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2026:-

(i) Fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa ni **asilimia 62.5** ya jumla ya fedha iliyotengwa ilihali katika kipindi hicho ilitakiwa mapokezi hayo yafikie **asilimia 66.6**

(ii) Fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa zimefika kiwango cha **asilimia 61** ya jumla ya fedha iliyotengwa ilihali katika kipindi hicho ilitakiwa mapokezi hayo yafikie **asilimia 66.6**

(iii) Fedha za mishahara zilizopokelewa zimefikia kiwango cha **asilimia 62.9** ya jumla ya fedha iliyotengwa ilihali katika kipindi hicho ilitakiwa mapokezi hayo yafikie **asilimia 66.6**

**Mheshimiwa Spika** uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2025 ulikuwa pungufu kwa **asilimia 4.1** ya lengo, ambapo Wizara ilipokea **asilimia 62.5** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hali hii inaashiria hatari ya kutokamilika kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2026 jambo linaloweza kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara endapo hatua hazitachukuliwa kabla ya kufikia mwisho wa mwaka wa fedha unaondelea.

### 2.2.3 Upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitengewa **Shilingi 41,887,535,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 27,870,710,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 14,016,825,000** ni fedha za nje.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Wizara ilipokea **Shilingi 20,377,278,432.09,** sawa na **asilimia 48.6** ya Fedha zilizotengwa, ambapo kiasi hicho ni fedha za ndani na hakukuwa na fedha za nje zilizopokelewa.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa kiasi hicho cha fedha za maendeleo kilichopokelewa kinajumuisha **Shilingi 4,000,000,000** kilichotolewa na Mheshimiwa Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni sehemu ya fedha alizotoa kwa ajili vijana kupitia wizara mbalimbali kiasi cha **Shilingi 200,000,000,000**. Mchanganuo wa fedha hizo za maendeleo ni kama invyoonekana katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Fungu 44 - Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| **Mtiririko wa fedha za Miradi ya Maendeleo hadi Februari, 2026** | | | |
|---|---|---|---|
| **MIRADI** | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2025/2026** | **Fedha Iliyopokelewa hadi Kufikia Februari, 2026** | **Asilimia ya Fedha zilizopokelewa** |
| Fedha za Ndani | 27,870,710,000 | 20,377,278,432.09, | 48.6 |
| Fedha za Nje | 14,016,825,000 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **41,887,535,000** | **20,377,278,432.09,** | **48.6** |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara 2026/2027*-Fungu 44 na usanifu wa Kamati




**Chanzo:** *Randama ya Wizara 2026/2027*-Fungu 44 na usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba hadi kufikia Februari 2026;

(i) Fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo imepatikana kwa **asilimia 48.6** ingawa katika kipindi hicho upatikanaji wake ulitakiwa kufikia asilimia 66.6

(ii) Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni wa **asilimia 73.1** na kuvuka lengo sawa na ongezeko la **aslimia 6.5.**

(iii) **Hakuna fedha za nje zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza Mheshimwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa **Shilingi 200,000,000,000** kwa ajili ya kuwezesha vijana Nchini. Sehemu ya fedha hizo **Shilingi 4,000,000,000** zilipelekwa Wizara ya Viwanda na Biashaa ili kuwezesha vijana katika Sekta ya Viwanda kupitia SIDO. Hatua hii inaonyesha dhamira ya kweli ya Serikali katika kukuza Uchumi wa vijana, kuhamasisha ubunifu, kujenga uwezo wa kujiajiri na kuanzisha biashara endelevu. Uamuzi huu ni chachu muhimu ya maendeleo ya vijana na unaendelea kuimarisha Dira ya Tanzania ya kujenga Uchumi shindani unaojumuisha wananchi wote hasa

vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa inayotegemewa zaidi.

### 2.2.4Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kufanya ziara ya kukagua utekelezaji wa Miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Katika ziara hiyo Kamati ilitembeleamiradi miwili inayotekelezwa chini ya Wizara hii. Miradi hiyo ni kama ifuatayo;-

**(a) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Vipimo na Viwango, Chuo cha Elimu ya Biashara-CBE**

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa ujenzi wa jengo la Vipimo na Viwango (Metrology Complex) lenye ghorofa 10 ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuboresha na kupanua miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ili kukidhi ongezeko la wanafunzi na kuimarisha mafunzo kwa vitendo. Mradi huu una thamani ya **Shilingi 26,398,228,771.45** ambapo unatekelezwa kwa awamu mbili, awamu ya kwanza inagharimu **Shilingi 10,398,228,771.45** na awamu ya pili inagharimu **Shilingi**

**16,000,000,000** ambazo ni mkopo kutoka Benki ya NMB. Ujenzi huu umefikia asilimia 93 na ulitakiwa kukamilika 23, Mei 2026. Mradi huu utakapokamilika unatarajia kuleta manufaa mengi ikiwa ni pamoja na kuongeza uwezo wa kuhudumia jumla ya wanafunzi 5,594 kwa wakati mmoja, kuimarisha mafunzo kwa vitendo na kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa chuo.

Aidha Kamati ilibaini kuwa zipo changamoto nyingine zinazokikabili chuo hicho ikiwemo uhaba wa miundombinu mingine kama vile hosteli ambapo Kamati ilielezwa kuwa ni **asilimia 3.57** tu ya Wanafunzi hukaa Hostel. Changamoto hii ya makazi inaleta kadhia ya makazi kwa Wanafunzi hususan Wanafunzi wa kike ambao kwa kiasi kikubwa huathiriwa na mwingiliano na Jamii.

**(b) Utekelezaji wa mradi wa Kituo cha Uhakiki Misugusugu- Kibaha. (Wakala wa Vipimo)**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Vipimo (WMA) ilianzisha mradi wa ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Uhakiki katika eneo la Misugusugu. Eneo hili lina ukubwa wa heka 2.4 na ujenzi wa Kituo hiki umekamilika na umegharimu **Shilingi 7,300,000,000.** Kuanzishwa kwa kituo hiki ni utekelezaji wa azma ya Serikali kusogeza huduma za vipimo karibu na wananchi, wadau wa kibiashara, pamoja na kuimarisha miundombinu ya uhakiki nchini.

Aidha, kituo kinalenga kufanya uhakiki wa matenki ya magari yanayosafirisha vimimikia, Mita mpya za Umeme na Dira za Maji kabla ya kufungwa kwa wateja, lengo la uhakiki huo ni kuhakikisha vifaa hivyo vinakidhi viwango vilivyowekwa na vinatoa matokeo sahihi ya matumizi.

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Vipimo inakabiliwa na changamoto mbili ikiwemo mwitikio hafifu kutoka kwa baadhi ya wazabuni wanaouza Mita za nishati ya umeme katika kutekeleza takwa la kisheria la kuhakikisha Mita hizo zinahakikiwa na Wakala kabla ya kuwasilishwa kwa taasisi nunuzi na Madai ya muda mrefu ya malipo ya huduma za uhakiki wa Dira za Maji kutoka kwa baadhi ya makampuni yaliyopewa zabuni ya Dira za Maji.

### 2.2.5Hali ya Uzingatiaji wa Ushauri Uliotolewa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na ushauri wa Kamati kuzingatiwa kwa sehemu kubwa, ipo sehemu ya ushauri ambayo utekelezaji wake haujakamilika. Mfano wa

ushauri huo ni kuhusu ukamilishaji wa mradi wa Magadi Soda-Engaruka na mradi wa Liganga na Mchuchuma. Maelezo ya mtoa hoja yanaonesha kuwa bado timu za majadiliano ya Mikataba ya Ubia na Kampuni zilizoshinda zabuni yanaendelea. Ushauri mwingine ni kuhusu upatikanaji wa umeme wa uhakika Viwandani ambapo mtoa hoja alieleza kuwa Serikali inaendelea na kupeleka njia maalumu za umeme (dedicated lines) katika maeneo ya viwanda. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa maagizo yenye muendelezo wa utekelezaji yaendelee kutekelezwa.

**SEHEMU YA TATU**

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 26 Machi, 2026 Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara – **Fungu 44** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi huo ulilenga kujihakikishia iwapo Mpango na Makadirio haya Pamoja na mambo mengine umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025- 2030.


### 3.1 Makadiriro ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, **Fungu 44 -** Wizara ya Viwanda na Biashara, inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya **Shilingi 104,122,530,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 78,049,345,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 26,073,185,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kiasi hicho ni ongezeko la **asilimia 10.88** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambayo ilikuwa ni **Shilingi 93,900,697,000**

**Jedwali Na. 3: Ulinganisho wa Fedha za Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na 2026/2027**

| Ulinganisho wa Bajeti Fungu 44 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **2025/2026** | **2026/2027** | **Ongezeko/ Pungufu** | **Asilimia** |
| Mishahara | 75,819,380,000 | 78,049,345,000 | 2,229,965,000 | 2.94 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 18,081,317,000 | 26,073,185,000 | 7,991,868,000 | 44.19 |
| **Jumla** | **93,900,697,000** | **104,122,530,000** | **10,221,833,000** | **10.88** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027-Fungu 44 na usanifu wa Kamati***




***Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027-Fungu 44 na usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo;-

(i) Makadirio ya fedha za matumizi ya kawaida kwa ujumla yameongezeka kwa **asilimia 10.88** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa fedha ulioisha.

(ii) Makadirio ya Fedha za Matumizi mengineyo (OC) yameongezeka kwa **asilimia 44.19** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa fedha ulioisha.

(iii) Makadirio ya fedha za Mishahara yameongezeka kwa **aslimia 2.94** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

**Mhesimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kuongeza Bajeti ya Wizara hii kwani kwa kufanya hivyo kutawezesha kukuza uchumi wa viwanda wenye ushindani, unaotegemea matumizi ya rasilimali za ndani, teknolojia, ubunifu na nguvu kazi yenye ujuzi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba sekta ya viwanda imepewa nafasi ya kimkakati katika Dira 2050 ya Taifa kama moja ya sekta za kipaumbele zinazochochea mageuzi makubwa ya Uchumi wa Taifa.


## 3.2 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ya Viwanda na Biashara **(Fungu 44)** inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya **Shilingi 33,690,103,000** sawa na punguzo la **asilimia 19.57** Ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka unaoisha kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambazo ni fedha za ndani na hakuna fedha za nje zilizotengwa. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 4.**

**Jedwali Na. 4: Ulinganisho wa bajeti ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na2 026 na 2027**

| Ulinganisho wa bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2025/2026 na 2026 na 2027 | | | |
|---|---|---|---|
| **MIRADI** | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2025/2026** | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2026/2027** | **Ongezeko/ Punguzo %** |
| Fedha za Ndani | 27,870,710,000 | 33,690,103,000 | 20.87 |
| Fedha za Nje | 14,016,825,000 | 0 | 100 |
| **Jumla** | **41,887,535,000** | **33,690,103,000** | **-19.57** |

***Chanzo:*** *Randama ya Wizara 2026/2027-Fungu 44 na usanifu wa Kamati*




***Chanzo:*** *Randama ya Wizara 2026/2027-Fungu 44 na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo:-

(i) Fedha za ndani kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maeondeleo zimepungua kwa **asilimia 19.57** ilkilinganishwa na bajeti ya mwaka unaoisha.

(ii) Hakuna fedha za nje za miradi ya maendeleo zilizopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, Makadirio ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yamepungua ikilinganishwa na Mwaka wa fedha 2025/2026. Hali hii inakwamisha mkakati wa Wizara unaolenga kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya Viwanda. Licha ya Wizara kutotenga fedha za nje. Kamati inaona ipo haja ya Wizara kuendelea kuandaa na kuwasilisha maandiko mbalimbali kwa washirika wa maendeleo ili kuhakikisha inapata fedha za nje zitakazosaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha Kamati inaona kuwa kutokana na upatikanaji wa fedha za nje za maendeleo umekuwa wa kusuasua ipo haja ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda ili kufikia adhma ya Tanzania ya Viwanda.

**SEHEMU YA NNE**

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia majadiliano ya kina baina ya Kamati na Wizara hii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ili kusaidia katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(a) Kutokana na ukweli kuwa Sekta ya Viwanda imepewa nafasi kubwa ya kimkakati katika Dira ya Taifa 2050 kama moja ya sekta za kipaumbele zitakazochochea mageuzi makubwa ya Uchumi wa Taifa jambo linalopelekea kuwa na uhitaji mkubwa wa fedha. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuona umuhimu wa kuiongezea Bajeti Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kutekeleza azma yake ya kuleta mageuzi ya kiuchumi.

(b) Hali ya upatikanaji wa fedha za maendeleo si ya kuridhisha. Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuna sababisha utekelezaji wa miradi

hiyo kusuasua, na mingine kutotekelezwa kabisa. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio.

(c) Kutokamilika kwa muda mrefu kwa mradi ya Liganga na Mchuchuma pamoja na mradi wa Magadi Soda Engaruka kumpelekea kuchelewa kwa maendeleo ya viwanda, kuendelea kutegemea bidhaa kama vile chuma, kemikali na malighafi nyingine kutoka nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi na za haraka katika kuhakikisha miradi hii inaanza kutekelezwa mapema iwezekanavyo. Kukamilika kwa miradi hii kutakuwa ni hatua muhimu katika kuimarisha Uchumi wa viwanda, kuongeza ajira na kutumia rasilimali za Nchi kwa maendeleo ya Taifa.

(d) Kutokuwepo kwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Nchini kunaathiri kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta ya Viwanda. Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuanzisha Mfuko huu. Aidha Kamati inashauri Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii kuchangia fedha kwenye Mfuko huu ili kuongezesha mtaji ikizingatiwa kwamba Mfuko huu unaweza kuwa nyenzo muhimu

katika kuimarisha uzalishaji, kuongeza ajira na kukuza Uchumi wa Taifa.

(e) Baadhi ya tozo katika biashara zinaathiri ushindani wa bidhaa za ndani dhidi ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi jambo linalopelekea kuongeza gharama za uzalishaji na kudhoofisha ukuaji wa viwanda vya ndani. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za serikali kufanya tathmini ya kina kuhusu tozo mbalimbali na athari zake katika biashara ili kubaini namna zinavyoathiri ushindani wa bidhaa za ndani dhidi ya bidhaa zinazoingizwa toka nje ya nchi. Hatua hiyo itasaidia kuboresha mazingira ya biashara, kuongeza ushindani wa viwanda vya ndani na kuchochea ukuaji wa Uchumi wa taifa.

(f) Kumekuwepo na malalamiko ya wananchi juu ya thamani halisi za matumizi ya huduma za muda wa maongezi na bando za intaneti. Kamati inasishauri Wizara kupitia Wakala wa Vipimo WMA kuanza jukumu la kuhakiki vipimo vinavyotumika kwenye muda wa maongezi na bando za intanet ili wananchi waweze kupata thamani halisi ya huduma wanazolipia.

(g) Kumekuwa na mwitikio hafifu kutoka kwa baadhi ya wazabuni wanaouza Mita za Nishati ya Umeme katika kutekeleza takwa la kisheria la kuhakiki mita hizo kwa Wakala wa Vipimo (WMA) kabla ya kuwasilishwa kwa taasisi nunuzi jambo linaloathiri usahihi wa Ankara (*Bill),* kuibua malalamiko ya walaji na kudhoofisha uadilifu wa mifumo ya mapato. Kamati inaishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kushirikiana na Wizara ya Nishati ili kuhakikisha Mita zote mpya za umeme zinawasilishwa kwa ajili ya kuhakikiwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo kabla ya kusimikwa kwa watumiaji.

(h) Changamoto ya lumbesa bado haijapata Suluhu la kudumu jambo linalopekea baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kuendelea kutumia mfumo huu na kupelekea kuwanyonya wakulima na kuikosesha serikali mapato. Kamati inaishauri Serikali kushirikisha mamlaka zote zinazohusika na vipimo ili kupata Suluhu ya kudumu. Usimamizi wa Pamoja utasaidia kubaini chanzo cha tatizo na kuweka mkakati Madhubuti ya kulidhibiti.

(i) Uwepo wa bidhaa feki sokoni unasababishwa na ukosefu wa udhibiti wa kutosha wa Mamlaka husika jambo linalopelekea Serikali kukosa mapato, kuathiri uwekezaji na kuleta athari kwa watumiaji. Kamati

inaishauri Serikali kuimarisha ukaguzi wa bidhaa mipakani na sokoni sambamba na kuziongezea nguvu mamlaka husika kwa kuwaongezea rasilimali watu na fedha ili kuimarisha ukaguzi nchi nzima.

(j) Serikali ihakikishe kuwa mifumo ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo inasomana ili kuwezesha mnyonyoro mzima wa uzalishaji na biashara unafuatiliwa kwa ufanisi. Hatua hiyo itasaidia serikali kupata taarifa sahihi kuhusu uzalishaji wa mazao, usindikaji wa viwandani, usafirishaji na mauzo ndani na nje ya nchi. Vilevile itasaidia kuongeza ufanisi wa usimamizi wa Uchumi na kuongeza mapato ya taifa.

(k) Tatizo la Biashara ndogo ndogo za Wazawa kufanywa na Raia wa Kigeni nchini kumeathiri kwa kiasi kikubwa ushindani kwa Wafanyabiashara Wazawa, kupungua kwa nafasi za ajira na kujiajiri na kushuka kwa ukuaji wa bidhaa za ndani. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha utekelezaji wa Sheria za bidhaa na uwezeshaji kwa kudhibiti vibali vya biashara kwa Wageni katika sekta ndogo ndogo za kibiashara.

(l) Uhaba wa Hosteli katika Vyuo vya Elimu ya Biashara (CBE)umesababisha asilimia 3.57 tu ya Wanafunzi katika vyuo hivi ndio hukaa hostel, jambo linalopelekea wanafunzi wengi kuishi nje ya Vyuo na kupelekea wanafunzi hususan wanafunzi wa kike ambao wengi wao wana umri chini ya miaka 18 kupata changamoto mbalimbali ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kwaajili ya ujenzi wa Hosteli ili kupunguza changamoto zinazowakabili Wanafunzi hao katika vyuo husika.

**SEHEMU YA TANO**

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kwa kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb | - | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb | | **M/Mwenyekiti** |
| 3. | Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo,Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Tauhida Galos Cassian, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Omar Marcus Msigwa, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb | - | Mjumbe |

11. Mhe. Kabula Enock Shitobelo, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Dkt.Rita Enerpher Kabati, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde Mb - Mjumbe
14. Mhe. Magreth Baraka Ezekiel, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Abubakar Alli Omari, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Kenneth Ernest Nollo, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Khalfan Issa Mohamed, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Khamis Hamad Yussuf, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Amour Seif Abdalla, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Khalid Mussa Nsekela, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Salum Khamis Salum, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb) - Waziri wa Viwanda na Biashara na Mhe. Dennis Lazaro Londo (Mb) – Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara na Taasisi zilizo chini ya Wizara

wakiongozwa na Katibu Mkuu Mheshimiwa Balozi Waziri Rajab Salum, akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu Bwana. Aristides Robert Mbwasi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard kwa kuwaongoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44), kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Deodatus Philip Mwanyika (Mb)

**MWENYEKITI WAKAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**

22 Mei, 2026